# KENYA NATIONAL EXAMINATION COUNCIL
# REVISION MOCK EXAMS 2016
## TOP NATIONAL SCHOOLS

**MOI GIRLS HIGH SCHOOL**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 3**
**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

**SCHOOLS NET KENYA**
Osiligi House, Opposite KCB, Ground Floor
Off Magadi Road, Ongata Rongai | Tel: 0711 88 22 27
E-mail:infosnkenya@gmail.com | Website: www.schoolsnetkenya.com

# MOI GIRLS SCHOOL - NAIROBI KCSE TRIAL AND PRACTICE EXAM 2016

**102/3**

**Karatasi ya 3**

**Mwongozo wa kusahihisha**

**Sehemu A -Ushairi.**

1. (a) Umbo la shairi.
   -Beti tano
   -Tarbia - lina mishororo minne katika kila ubeti.
   -Mtiririko - kina cha kati na mwisho kinatiririka
   -Mizani ni 16 katika kila mshororo (8 katika
   -ukwapi, na 8 katika utao)
   -Lina kibwagizo

   (b) Jazanda aliyotumia mshairi ni;
   -Mti - bara la Afrika
   -Vitawi - nchi za Afrika
   -Maradhi - Jamii za Kiafrika kuathiriwa na

   ukoloni na kuuendeleza.

(b) "Kutibu si masihara kwateka kutuma nguvu"Anamaanisha kuwa ili kuutibu ugonjwa huu ni lazima mtu ajikaze / atie bidii wala si mchezo.

(c) Inkisari
Kutuma – kutumia
tanzuze - tanzu zake

(d) Maana ya kibwagizo.
Ni kuwa ili kuutibu ugonjwa lazima mtu aanzie shinani, maana akitibu dalili tu ugonjwa hautapona.

**(e) Maana ya maneno.**

i) Kuporapora - kupigapiga.

ii) Isombe - ichukue, ibebe

iii) Sangara - mdudu mkali

iv) Miparura - miti yenye miiba

v) Mishughulivu - miti inayotaabika kutafuta chakula.

**<u>Sehemu ya B - Riwaya</u>.**

- Askari badala ya kulinda usalama wanampiga mama Imani vibaya.
- Nasaba Bora anahusiana kimapenzi na msichana mchanga Lowela.
- Nasaba Bora badala kuwajibikia umaskini wa raia, anaendelea kuchukua kidogo cha walonacho
- Majisifu kutowahudumia watoto wake ambao wana mahitaji maalumu, analalamika tu.
- Fao kuhusiana kimapenzi na wanafunzi wake.
- Nasaba Bora anaendeleza ufisadi badala ya kuupinga, anawahonga polisi, makarani wa mahakama na mahakimu ili kumtia Yusuf gerezani.
- Nasaba Bora anaamrisha kufungwa kwa Amani na Imani ilhali anajua hawakumwua mtoto.
- Nasaba Bora anapuuza kuwachanja mbwa wake. Mmoja wa mbwa hao anamwuma DJ na kusababisha ugonjwa. Nasaba hamwonei huruma, anasema DJ anastahili hayo.
- Viongozi wanawatelekeza raia kwa magonjwa, ujinga na njaa mf. Matuko Weye.
- Wauguzi katika zahanati ya Nasaba Bora kukataa kumtibu Uhuru - baadaye anakufa.
- Nasaba Bora anafuja hela zilizotengewa kujenga hospitali. Badala yake anajenga zahanati.
- Nasaba Bora kutohudumia Bi. Zuhura ipasavyo.
- Majisifu kumwibia Amani mswaada wake wa Kidagaa Kimemwozea.
- Nasaba Bora kumpiga Amani kwa kushuku kuwa ana uhusiano na mkewe.
- Nasaba Bora kusababisha vifo vya Mwinyi Hatibu na Chichiri Hamadi. *zozote 10 x 2 = 20*

2. (a) Mashaka alijiuliza.

    Katika uwanja wa Uhuru kuadhimisha
    Siku ya wazalendo
    Alimrejelea Matuko Weye. *4 x 1 = 4*

    (b) (i) Balagha - Anafikiri sherehe hizi ni za watu wenye kichaa kama yeye?

(ii) Kinaya - Matuko Weye si mwendawazimu hasa kwani alitambua uovu wa Nasaba Bora.

*2 x 2 = 4*

(c) **Ni mwendawazimu kwa sababu.**

- Ni mzee aliyekuwa hana mke wala watoto.
- Alivaa kaptura juu ya suruali zote zikiwa mararu.
- Hakumiliki chochote na aliweza kulala popote.
- Hakuvaa viatu tangu atoke vitani Burma kwani alikuwa mwehu.
- - Aliboboja maneno ovyo ovyo na alikula vyakula vya kupolea.
- Alipopewa chakula na kitoweo, alikula kitoweo kwanza kisha akala chakula, km - alikula mboga kisha akala sima
- alikula kuku kisha akala chapati.
- Alipenda kupiga kwata na kusema “mark - time”
- “about turn” na ‘left-right’ alipokumbuka miaka yake ya nyuma jeshini.
- Alisimulia vituko na visa vya vitani ambavyo vilikuwa nusu kweli na nusu mfundiro vya akili yake chakaramu.
- Anarejea korokoro alikopelekwa kama ikulu alipoamshwa na kelele za askari, Imani na Amani.
- Pia anajirejelea kama Mtukufu Rais.
- Anamtusi askari aliyemwita wazimu
- Alipotolewa seli alikataa kutoka na kusema kuwa
- kama Rais anawaamuru askari wawaachilie Imani na Amani.
- Alipopewa chakula alikula na kuondoka bila shukrani. *`6 x 1 = al 6*

(ii) <u>Matuko Weye anaweza kuchukuliwa kama asiye nawazimu kwa sababu</u>.

- Alifaulu kupanda jukwaani na kuchukua kipaza sauti bila kutambulikana.

- Hotuba yake inadhihirisha kuwa anafahamu wanavyonyanyaswa na Mtemi Nasaba Bora na anafahamu maovu anayofanya.

- Pia katika hotuba yake anawachochea watu kwa kusema wanataka Mtemi Nasaba Bora aondoke madarakani na anamtahadharisha Mtemi asione kwenda mbele kurudi nyuma si kazi.

- Alifanya kazi za sulubu ili kujikimu maishani.

- Alisema kuwa anamjua sana Amani na hangeweza kudhuru hata nzi na angeweza kumfanya waziri wa Ufisadi na Magendo.

- Anajua kuwa nchi yao ilitawaliwa na watu wa kutoa kitu kidogo ili wapewe madaraka ndipo anamwambia

- Amani kwa kinaya kuwa akitoa kitu kidogo atamfanya waziri.

- Alishtuka sana alipoambiwa na Amani kuwa amepelekwa seli kwa mauaji na kushikilia kuwa hawezi kuua. Anataka Amani aachiliwe huru na badala yake ashtakiwe yeye kwa haya mauaji.

- Anamtaka Imani aolewe na azae watoto watakaoikomboa Tomoko kutoka kwa mkoroni mweusi.

- Anasema kuwa ni afadhali mkoloni mzungu kuliko mkoloni mweusi kwa sababu anawadharau wenzake vibaya sana.

- Anawaambia askari kuwa mtu mwenye akili timamu hangewatia mbaroni watu wema kama Imani na Amani.

- Anashikilia kuwa mahakama ndiyo yenye hatia kwa kuwakamata Imani na Amani ambao hawakuwa na hatia.

- Anamwambia askari kuwa mama aliyemzaa aliwakosea wanadamu. Pia anamkumbusha askari kuwa hata yeye na Mtemi wao watakuja kuongezewa jina marehemu siku moja.

- Anawalaumu askari kwa kumshika na kumlaza njaa kisha kumwachilia kabla ya kumfikisha mahakamani.

- Anamwambia askari kuwa hata wakimuua watazaliwa Matuko wengine watakaoendelea na harakati za ukombozi kutoka pale alipoachia ili waikomboe nchi yao kutoka kwa mkoloni mweusi katika ukombozi wa pili.

- Alipopewa kasri lililokuwa la Majununi baada ya mapinduzi alifurahi mpaka jina la mwisho.

*6 x 1 = al 6*

4. **Mstahiki Meya - Timothy Arege.**

(a) (i) Siki anazungumza na Tatu.
(ii) Wako katika zahanati (ofisini mwa Siki)
(iii) Ni baada ya mgomo kutokea na Siki anamshauri Tatu kuendelea kutekeleza mabadiliko kwa njia ya amani.*al 4*

(b) Msemewa ni Tatu.
Sifa.

i. Mtetezi wa haki.

ii. Jasiri

iii. Mzalendo

iv. Mshauri

v) Mwanamapinduzi. 4 x1 = 4

(c) (i) Vitisho
(ii) Uongo
(iii) Sheria kandamizi - riot act, mayors act.
(iv) Propaganda - nyimbo za kizalendo.
(v) Mfumo wa tenga - utawale.
(vi) Mapendeleo.
(vii) Vyombo vya madola (askari)
(viii) Ubaraka na ubarakala (ukaragosi) *6 x 2 = 12*

5. Mstahiki Meya.

- Kuongoza nchi kwa udikteta - wafanyakazi walipogoma alikataa kukutana na viongozi.

- Kutumia uongo - Alidanganya kuwa ameagiza dawa

- na zingefika katika muda wa siku sita. Watu waliendelea kufa na Nesi Waridi akaacha kazi.

- Kutozingatia ushauri mzuri - Alipuuza ushairi wa Diwani III na Daktari Siki. Alifanya maamuzi mabaya

- yanayoangusha utawala wake.

- Kutumia mbinu ya tenga utawale. Kwa kutoa nyongeza ya mishahara kwa mapendeleo. Wasioridhika waliandaa migomo, wakasusia kusafisha mji na wageni wakakatiza safari yao.
- Kutowalipa watu kwa wakati ufaao - Migomo inaandaliwa.
- Madiwani kutolipa kodi. Waliolipa ni wale wa tabaka la chini wenye mapato madogo. Uchumi wa baraza
- unazorota.
- Kutumia askari kuwatesa wananchi – Wananchi waliumia na mwishowe wakaungana kupambana na meya kupitia kwa migomo.
- Kutumia vitisho- Alitisha kuwafuta kazi wafanyakazi waliogoma. Hili liliwatia motisha zaidi ya kuandaa
- migomo iliyoangusha utawala.
- Kutumia vibarakala - Diwani I and II walimshauri vibaya, nchi ikawa kwenye matatizo na utawala wake ukaporomoka.
- Kuuza fimbo ya meya - ingekuwa hasara kwa mji pamoja na hatari ya kugunduliwa baadaye wizi huo.
- Kumtumia mhubiri - Alijificha ndani ya dini na kumlipa mhubiri pesa nying hivyo kufilisisha baraza.
- Kutumia propaganda - Kuwachezea wananchi nyimbo za uzalendo. Hatimaye walichoshwa na maneno
- matupu walitaka vitendo.
- Kutumia sheria kali za kujilinda (kv. mayor’s act, riotact) wananchi waliumia na wakaandaa migomo ya kutetea haki zao. *10 x 2 = 20*
-

6. **Damu Nyeusi.**

(a) Yalisemwa na mmoja wa wachuuzi.
Alimwambia Christine
Ni katika kituo cha matatu
Christine alikuwa ametoka ofisini mwa Peter/
Kumjuvya jinsi alivyoavya mimba.
Alikuwa safarini akielekea kwao. *4 x 1*

(b) Sadfa - Ni sadfa kuwa Christine ameavya mimba ilhali mchuuzi anamwambia awaonee watoto huruma.

*kutaja 1 maelezo 1 = 2*

(c) (Maudhui ni ukatili)

- Wauguzi ni katili - Margret anamsaidia Christine kuavya mimba.
- Matajiri - Huwaingiza wasichana wadogo katika mapenzi na kuvuruga masomo yao. mf. Peter alitembelewa na Christine kila Ijumaa.
- Peter anawapunja wafrika kwa kununua samaki zao bei ya chini.
- Waajiri waliwakemea wafanyakazi waafrika vikali - Peter aliwatolea wafanyakazi amri kali.
- Waajri walilipa wafanyakazi mishahara duni. *3 x 2 = 6*

(b) Sifa za Christine.

- Mpenda anasa - Anatamani kuwa na uhusiano wa kimapenzi na matajiri. Alitoka chuoni kufuata Peter
- kwa starehe na anasa.
- Anashawishika haraka- Anapoambiwa na Zac kuwa Peter alimpenda alikubali na kuanza kumtembelea.
- Mwoga - Hana ujasiri wa kumweleza Peter kuhusu hali yake ya uja uzito.
- Mzinifu - Anashiriki mapenzi na Peter ilhali hawajaoana.
- Katili - Anaavya mimba.
- Mkosa maadili - Anamruhusu Peter kumbusu hadharani.
- Mwenye majuto - Anajuta baada ya kuavya mimba.
- Mwenye mapuuza - Anapuuza ushauri wa Dorothy kuhusu uhusiano wake na Peter.
- Mnafiki - Awali alikuwa mkristo aliyeokoka lakini vitendo vyake vilikuwa kinyume na maadili. *4 x 2*

7. Hadithi Fupi.
   Mwiba wa kujidunga.

- Samaki wa Nchi za Joto - Christine kujiingiza katika uhusiano na Peter akiwa chuoni kisha anapata mimba,
- kuiavya na kukosa kuolewa.
- Maeko - Jamila kuendelea kukaa katika ndoa iliyojaa mateso kutoka kwa mumewe licha ya kuwa mumewe
- habadili tabia.
- Kanda la usufi - Sela kujiingiza katika mapenzi akiwa shuleni kisha kupata mimba na kufukuzwa shule.
- Masazu kushiriki mapenzi akiwa shuleni kisha kukosa kufaulu mtihani na kuishia kufanya kazi duni.
- Gilasi ya mwisho makaburini - Semkwa na wenzake kuonywa kuhusu kwenda katika baa ya makaburini kisha wanapoenda wanavamiwa na majambazi - vizuu.
- Ndoa ya samani - Amali kumkataa Abu alipokuwa maskini kisha anaachwa hoi wakati wa arusi.
- Mke wangu - Msimulizi kumchagua Aziza akidhani atamvumbika, mkewe anamgeuka.
- Mwana wa Darubini - Mwatela kumbaka Kanada kisha anapozaa anamnyang'anya mtoto kumtorosha kisha Kananda anamtafuta hadi anampata na kurudiana na mwanawe.
- Mizizi na matwi - Bi. Kudura kumwacha mwanawe mchanga pipani kisha kuteseka akimtafuta, miaka mingi
- baadaye.
- Tazamana na mauti - Lucy kuwania kwenda Uingereza kwa vyovyote vile na kwenda kufia huko.
- Kikaza - Wanakijiji kuendelea kuchagua viongozi wasisotahili na kuumia kila wakati.

**<u>Fasihi simulizi.</u>**

8. Maghani ni utungo wa kishairi ambao hutongolewa kwa kutumia sauti iliyo kati ya uimbaji na uzungumzaji.
   (b)

   - <u>Vivugo</u> ni ushairi wa kujisifia unatungwa papo hapo na fanani mwanaume.
   - <u>Tondozi</u> - Utungo wa kutukuza watu, wanyama, vitu kama magari, miti, milima n.k

- <u>Pembezi</u> - ni aina ya tondozi ambayo imekusudiwa kusifia watu na aina fulani katika jamii kutokana na matendo yao au mchango wao katika jamii.

- <u>Rara</u> - utungo wa kishairi wenye ubunifu mkubwa unaokusudiwa kusisimua hadhira.

*Hoja 4 x 2 = 8*

(c) Maana ya ulumbi .

Uhodari wa kuzungumza au kuiga mazungumzo
kwa usanii na uhodari mkubwa. *al 1*

(d) <u>Sifa za mlumbi.</u>

-Mwenye ujuzi wa utamaduni, desturi, mila na sheria za jamii (mzingiro) ujuzi mkubwa wa maisha.
-Ufundi wa kutumia lugha, semi, mafumbo n.k
-Uwezo wa kutumia mbinu mbalimbali za kuwasiliana mfano, nyimbo, ushairi n.k
-Umahiri wa kughani, kusema kwa mfululizo na mwendo wa kasi.
-Kutumia sauti inayosikika bila shida.
-Ufundi wa kutumia kunga za maswali.

(e) <u>Umuhimu wa ulumbi.</u>

-Kipimo cha kimsingi cha mtu kuteuliwa kama viongozi.
-Njia maalum inayotumiwa na jamii kupitisha ujumbe muhimu.
-Njia ya kudumisha utamaduni na thamani za kitamaduni kwa kuzionea fahari.
-Ni kitambulisho muhimu kwa jamii na wanajamii.